

Mapesbury Clinic

Nasaha kwa wakimbizi wa jinsi tofauti

020 7 644 6250

www.mapesburyclinic.org.uk

Maelezo

Clinic ya Mapesbury ni mipango inayo ongoza na inakusudia kuwapatia nasaha na msaada wa matibabu ukamilifu kwa wakimbizi na waombi wa makaazi (ya amani). Nasaha na matibu yanapewa na watu waliosomea na wana mafunzo ya juu kutoka mila na mazoezi tofauti, wengi wao wenyewe walikuwa wakimbizi.

Pia msaada huu inawapatia fursa watu wa nasaha waliyekuwa wakimbizi na wengine waliye na masomo yanayohitajika na wanazungumza lugha mbali mbali vizuri nafasi ya kutibu. Hizi nafasi zinasaidiwa kwa maangalizi ya kila wakati na njia ya kubata masomo zaidi.

Azimio

Azima (kusudi) yetu ya kwanza ni kuwapa wakimbizi na waombi wa makaazi (wa amani) msaada wa nasaha na matibabu inayo wafaa kwa lugha na mazoezi zao.

Kwa Ajili Ya Nani?

Msaada huu ni wa bure kwa wakimbizi, pamoja na waombi wa makaazi (amani) na watu ambao wako mbali na nchi zao wenye umri wa miaka 18 na kuzidi wanaokaa katika mmoja ya mitaa wa London. Hata hivyo, wakimbizi na waombi wa makaazi (amani) wanaotoka nje ya London hawatonyimwa msaada huu. Inategemeya hali, Ikihitajika, msaada wa nauli huenda ukapatikana.

Msaada Tunayotowa

- Clinic ya Mapesbury inatoa msaada wa nasaha na matibu ukamilifu kwa mazoezi na malugha tofauti kama Kiarabu ya (Kazkazini ya Africa, Mashariki Kati na aina zote), Kifaransi, Kifarsi, Kispanish, Kibosni, kitamil, lugha ya Serbo-Croat, Kikurdish, Kialbani, Kisomali, Kiturkish na Kingereza.

Kadiri na idadi ya lugha zinazotumika kwenya Clinic ina badilika na kuongezeka baadhi ya wakati. Tafadhali ulizia.

- Pia tunawapa msaada wa kutetea na kupewa maarifa kwa watumiaji wa Clinic kwa mambo kama ya uhamiaji, msaada wa pesa, pahala pa kukaa, na msaada wa makaazi (kwa amani). Pia tunawapeleka watumiaji wetu kwa kushauriwa na wenye ujuzi na kwa kutetewa kwenye hali hizi na nyenginezo. Tafadhali fahamu yakwamba msaada huu ni kwa ajili ya watu wanaotumia nasaha ya Clinic tu.
- Tunashirikiana na mashirika mengine ili zipatikane njia za misaada mengine inayohitajiwa na watumiaji wetu.

Unafika Vipi

- Watu wanaweza kuja wenyewe au wanaweza kuletwa na mataktari wao (GPs), wana afya ama wafanyi kazi wa jamii. Pia Clinic itakubali watu wanaoletwa na mashirika ya umati na yaliojitolea. Mafomu ya kujaza zinaweza kupatikana katika Clinic, kutoka kwenye ukurasa wetu wa Internet, au tunaweza kupokea mafomu mengine yaliyojazwa kama inavyotakiwa.
- Mafomu yakifika tu, watumiaji wataarifiwa. Baadae inaweza kufika miezi mitatu kabla ya kuarifiwa lini utaulizwa maswali.

- Haya maswali yatatuwezesha kufahamu msaada wa nasaha au matibabu ambayo itakufaa na tunaweza kukupatiya. Kama Nasaha haifai, mtumiaji na mtu ambaye aliemleta watajulishwa kwa maandishi.

Baada ya mkutano (wa maswali)

- Nasaha au matibabu yataanza mara tu patapopatikana nafasi. Mpaka hapo, watu watakuwa kwenye orodha ya kuongojeya na wataambiwa muda utakao kuwa.
- Watumiaji wataweza kutumiya msaada wa kutetewa na Clinic na kupewa maarifa ikiwa wanahitaji misaada mengine kama zile zinazohusu makaazi.
- Nasaha inatolewa kwa wiki mara moja, muda wa mara kumi na mbili kwa kawaida. Ikibidi nasaha ama tibabu yanaweza kutolewa kwa muda mrefu lakini inategemeya hali ya watu.

Misaada ambayo hatutowi

- Clinic ya Mapesbury haitowi misaada ya ghafla; watumiaji wataangiliwa baada ya kufanya miadi tu.
- Msaada hii haifai kwa wagonjwa wanayo ugonjwa wa akili au hivi sasa wana matatizo ya kutumia zaidi madoroga (madawa ya unga) ama kunywa ulevi. Wenye matatizo haya watapelekwa kutafuta misaada kwa wana maarifa wengine wakipatikana, wapewe shauri inayo wafaa.

Siri

Maandishi na maelezo mengine tulizopata kwa watumiaji wetu yatawekwa kwa mahala pa siri sana kwa maaila, marafiki na watu wengine wote wasijuwe. Tutaweza kuwaonyosha watu wengine baada ya kupata ruhusa ya maandhishi kutoka kwa mtumiaji aliehusika tu. Ikibidi twende kinyume na sharia (ya siri) maelezo yatatolewa mwanzo wa mkutano wa nasaha.

Wakati wa kufunguwa na maswali

Kuletwa

Wafanyi kazi wanapatikana Jumanne mpaka Ijumaa kutoka saa 10:00 asubuhi mpaka 5:30 alasiri na Jumamosi kutoka 10:00 asubuhi mpaka 2:00 adhuhuri.

Nasaha

Pia misaada inaweza kupatikana baada ya afisi kufungwa. Wenye vilema wanaweza kuingia ndani ya jengo letu na magari yao.

Maswali

Ukihitaji habari nyengine au una maswali piga simu kwa Klinik 020 7644 6250 au angalia ukurasa wetu wa Internet www.mapesburyclinic.org.uk

Utatupata Vipi ?

Kituo cha train karibu: Queen's Park (Layn ya Bakerloo)

Kituo cha Rail karibu: Brondesbury Park & Queen's Park
(Layn ya Silverlink)

Mabasi nambari: 6, 36, 187, 206, 316

Hamuna mahala ya kuweka magari.
Karibu na sisi unaweza kuweka gari (kulipa) kwa muda.

Clinic ya Mapesbury

20 Lonsdale Road, Queen's Park, London NW6 6RD

Tel: 020 7644 6250

Fax: 020 7644-6241

Email: clinic@minstercentre.org.uk

Ukurasa wetu wa Internet: www.mapesburyclinic.org.uk